Maswali

1. Nani alikuwa mfalme wa Waisraeli?
2. Mbona watu hawakuridhika na uongozi wa wana wa Samweli?
3. Waisraeli waliambia Samweli kwamba wanataka nini?
4. Mbona walitaka binadamu awe mfalme wao?
5. Samweli alijisikia namna gani
6. Mungu aliambia Samweli nini?
7. Nani alichaguliwa kama mfalme mpya?
8. Sauli alikuwa mtu wa namna gani?
9. Mbona Sauli alienda kwa mji wenye Samweli alikuwa akiishi?
10. Nani alipaka Sauli mafuta awe mfalme wa Israeli?

Majibu

1. Mungu alikuwa mfalme wa Waisraeli.
2. Wana wa Samweli wawili walikuwa waovu tena walichukua hongo.
3. Waisraeli walitaka binadamu awe mfalme wao
4. Walitaka binadamu mwenye watamuona tena awaongoze kwenda vita
5. Samweli aliona vibaya sana.
6. Mungu alisema, Waisraeli hawakuwa wamekataa Samweli. Walikuwa wamekataa Mungu.
7. Sauli alichaguliwa kuwa mfalme mpya.
8. Sauli alikuwa mrefu na zura nzuri. Alikuwa na nguvu tena hotari wa kupigana.
9. Sauli alikuwa anatafuta punda wenye baba yake alikuwa amepoteza.
10. Samweli alipaka Sauli mafuta awe mfalme wa Israeli.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 2

57 Waisraeli wanataka mfalme

Kwa Biblia

1 Samweli milango ya 8, 9 na 10

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Waisraeli walitaka mfalme badala ya kuamini Mungu awatawale. Tukiwa na shida lazima tukumbuke kwamba, hata kama Mungu haonekani, ako karibu na sisi na atatusaidia kila wakati

Somo

Mungu alichagua Waisraeli kuwa watu wake wakipekee. Hapo zamani Mungu alikuwa amewasaidia Waisraeli watoke Misri. Aliwaongoza na kuwalinda wakati wote wa safari ya jangwani. Tena Mungu aliwasaidia kupiga na kushinda nchi ya Kanaani. Mungu alikuwa Mfalme wa Waisraeli walipokaa na kutulia kwa hiyo nchi. Mungu aliwawekea waamuzi kuwafundisha sheria zake. Kwa miaka mingi, waamuzi walisaidia kusimamia Waisraeli. Lakini Mungu alikuwa ndiye mfalme wao. Samweli alikuwa mwaamuzi wa mwisho. Alikuwa kiongozi wa nguvu.

Samweli alipokuwa mzee hangeweza kufanya kazi nyingi. Hangeweza kuamua kesi za ugovi zote. Samweli alifanya wana wake wawili wamsaidie kazi. Lakini wana wa Samweli walikuwa waovu.

Waisraeli waliamua kwamba hawataki Mungu awe mfalme wao tena. Walitaka binadamu awe mfalme wao. Walitaka mfalme mwenye watamuona. Walitaka mtu wakuwaongoza wakiende kwa vita. Waisraeli waliambia Samweli kwamba wanataka mfalme mpya.

Samweli aliona vibaya sana wakati Waisraeli walipouliza mfalme mpya. Samweli aliambia Mungu maneno yenye Waisraeli walisema. Mungu aliambia Samweli asione vibaya. Mungu aliambia Samweli kwamba Waisraeli hawajamkataa yeye kuwa mfalme wao. Walikuwa wamekataa Mungu. Mungu alisema atawaachilia wawe na mfalme.

Samweli aliambia Waisraeli kwamba mfalme mpya atawafanyia vitu vingi vyenye hawatapenda. Aliwambia, “Mfalme atachukua wana wenu kuwa askari wake. Atachukua binti wenu kuwa wapishi wake. Atachukua mashamba yenu mazuri ya mizabibu na ya mizeituni yawe yake. Nyinyi wote mtakuwa watumishi wake.” Lakini Waisraeli walikuwa wameamua wanataka mfalme. Hawakusikiliza hadhari ya Samweli. Mungu aliambia Samweli kwamba Waisraeli watakuwa na mfalme.

Mungu alichagua mfalme mwenye watu wote watapenda. Alikuwa wa zura nzuri na mrefu. Alikuwa na nguvu. Alikuwa hodari kwa vita. Jina lake aliitwa Sauli. Alikuwa mwana wa Kishi wa kabila la Benyamini.

Kishi alipoteza punda zake. Alituma Sauli na mtumishi waende kutafuta. Sauli walienda kila pahali lakini hawakupata punda. Halafu wakaenda kwa mji wenye Samweli alikuwa akiishi. Sauli na mtumishi wake waliamua kuuliza Samweli penye punda walienda.

Siku moja kabla Sauli afike, Mungu alizungumza na Samweli. Mungu aliambia Samweli kwamba, kesho Sauli atakuja mjini. Sauli ndiye mtu Mungu alikuwa amemchagua kuwa mfalme mpya. Mungu aliambia Samweli ampake Sauli mafuta ili awe mfalme wa Waisraeli.Sauli alipofika mjini, Samweli alimwambia kwamba punda wamepatikana.

Halafu Samweli alikaribisha Sauli na mtumishi wake wakae ili washiriki kwa karamu yenye itakuwa mjini. Sauli alienda kwa karamu . Samweli alimpa kiti pahali pa heshima. Sauli alipewa chakula kizuri zaidi. Sauli na mtumishi wake walikaa kwa Samweli.

Asubuhi iliyofuata Samweli aliita Sauli. Samweli alipaka Sauli mafuta ili awe mfalme wa Waisraeli. Samweli aliambia Sauli ishara ya kuonyesha kwamba Mungu alikuwa amemchagua kuwa mfalme. Samweli alimwambia wale watu atakao kutana nao njiani akienda nyumbani. “ Kwa uwanda wa Tabori utakutana na watu watatu wanaenda Betheli, mtu mmoja atakuwa na mbuzi, mtu mwingine atakuwa na mikate mitatu na watatu atakuwa na chupa ya divai. Watakupea mikate miwili.”

“Kwa kambi ya Wafilisti utakutana na kikundi cha manabii wako na mitambo ya muziki. Watatoa unabii na hata wewe pia utatoa nao.” Sauli alipotoka kwenda nyumbani, alipata kila kitu vile Samweli alitabiri.

Samweli alikusanya Waisraeli wote pamoja. Akawaonyesha mfalme wao. Sauli alikuwa mrefu tena mzuri wa umbo. Alikuwa kwa kichwa na mabeka mrefu kuliko Waisraeli wengine wote. Waisraeli walifurahia mfalme wao mpya. Walipiga kelele wakisema, “Mfalme aishi milele.”

Sauli alikuwa ndiye mfalme mpya wa Israeli. Alikuwa ndiye watu wa Israeli waliona. Sauli alikaa pamoja na watu wake na aliwaongoza kupigana na adui wao. Lakini mfalme wa kweli wa Israeli alikuwa Mungu. Sauli alitawala kwa niaba ya Mungu.